Nambari ya Mtahiniwa ......................................

S.M.Z

BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

MTIHANI WA DARASA LA NNE

123 SAYANSI

MUDA SAA 2:00 JUMANNE 15 DISEMBA, 2020 ASUBUHI

MAELEKEZO KWA WATAHINIWA

1. Mtihani huu una sehemu MBILI (2) A na B.
2. Jibu maswali YOTE katika sehemu A na B.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Majibu YOTE yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.
5. Tumia kalamu nyeusi au ya buluu kwa kuandikia na penseli kwa kuchorea tu.
6. Simu za mkononi na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi ndani ya chumba cha mtihani.

| KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI | | |
|---|---|---|
| SWALI | ALAMA | SAHIHI YA MSAHIHISHAJI |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |
| 9. | | |
| 10. | | |
| JUMLA | | |

Mtihani huu una kurasa 8 zenye maandishi



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Nambari ya Mtahiniwa ......................................

SEHEMU A: (ALAMA 40)

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.

1. Chagua jawabu sahihi kisha andika herufi yake kwenye jadweli Hapo chini ya maswali.

i. Mswaki kazi yake ni
   A. Kunawia uso
   B. Kufulia nguo
   C. Kusafishia meno
   D. Kusafishia choo

ii. Vyanzo vya maji ni
   A. Mvua, mto na kisima
   B. Chemchem, mfereji na kisima
   C. Bahari, mto na tenki
   D. Kisima, shimo na chemchem

iii. Miongoni mwa aina za misitu ni
   A. Misitu ya moja kwa moja
   B. Misitu mizuri
   C. Misitu ya asili
   D. Misitu inayovutia

iv. Moja kati ya vyanzo vya hewa ni
   A. Maji
   B. Feni
   C. Dirisha
   D. Kiyoyozi

v. Mlo wenye virutubisho vyote vya chakula huitwa
   A. Vyakula mchanganyiko
   B. Chakula bora
   C. Matunda na mboga mboga
   D. Mlo kamili

JAWABU

| i | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

2. Andika kweli au sikweli katika maelezo yafuatayo kwenye jadweli Hapo chini.

i. Tumia gongo bichi kumnasua aliyenasa katika umeme.

ii. Mimea isiyotoa mauwa hai na tunda halisi.

iii. Wanyama wasiofugwa huhitaji uangalizi wa binadamu.

iv. Udongo ni tabaka la juu la ardhi.

v. Utupaji taka kwenye vyanzo vya maji hutupatia maji safi na salama.

JAWABU

| i | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

3. Oanisha maelezo ya kifungu A kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kifungu B. Andika herufi tu kwenye jadweli hapo chini.

| KIFUNGU A | KIFUNGU B |
|---|---|
| i. Majani yake huwa membamba na yenye ncha | A. Muembe na mchungwa |
| | B. Mboga |
| ii. Hutengeneza chakula kwa msaada wa jua, hewa na maji | C. Kitunguu maji na kabichi |
| | D. Husababisha mvua |
| iii. Faida za misitu | E. Mchaichai na mua |
| iv. Mimea inayohifadhi chakula kwenye majani | F. Majimbi |
| | G. Mimea |
| v. Hutoa matunda na mbegu | H. Mchaichai na muhogo |

JAWABU

| i | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

4. Jaza nafasi zilizoachwa wazi. Tumia maneno yaliyomo kwenye kisanduku hapo chini ya maswali.

i. Kinakuwemo kwenye kisanduku cha huduma ya kwanza na hutumika kusafishia kidonda____________________.

ii. Tunapohisi __________________________ tunakunywa maji.

iii. Ufupisho wa virusi vya Ukimwi ni _______________________.

iv. Gongo refu linalochongwa vizuri na kuingizwa kwenye Jembe ni__________________________.

v. Mtaro ni msingi ambao hutumika kupitisha maji _______________.

| | | | |
|---|---|---|---|
| pamba, | VVU, | kiu, | mpini, |
| machafu, | UUV, | kitambaa, | mshipi. |

SEHEMU B: (Alama 60)

Jibu maswali YOTE kwenye sehemu hii.

5. a) Andika madini mawili (2) yanayopatikana kwenye udongo.

i. ____________________________________________________

ii. ____________________________________________________

b) Bainisha vitu viwili (2) vinavyotengenezwa kwa njia ya ufinyanzi.

i. ____________________________________________________

ii. ____________________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

c) Taja viumbe viwili (2) vinavyoishi kwenye udongo.

i. ____________________

ii. ____________________

6. a) Nini maana ya kipima joto?

____________________

____________________

____________________

b) i. Kuna aina ngapi za kipima joto?

____________________

ii. Zitaje

____________________

____________________

c) Bainisha njia kuu tatu (3) za kusafiri kwa joto.

i. ____________________

ii. ____________________

iii. ____________________

7. a) Nini maana ya kipigi?

____________________

____________________

____________________

____________________

____________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

b) Kipigi kinafanyika vipi?

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

c) Taja rangi zote zilizomo kwenye kipigi.

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

8. a) Nini maana ya mwangwi?

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

____________________________________________

b) Orodhesha vitu vinne (4) vinavyosababisha kufanyika kwa mwangwi.

i. ____________________________________________

ii. ____________________________________________

iii. ____________________________________________

iv. ____________________________________________

c) Andika sehemu mbili (2) ambazo mwangwi hutumika.

i. ____________________________________________

ii. ____________________________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

9. a) Nini maana ya uvunaji wa maji?

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

b) Kamilisha jadweli lifuatalo kwa kuchagua maneno sahihi yaliyomo ndani ya mabano.

( uzi, maji, maziwa, mbao, upepo )

| VITU YABISI | VIMIMINIKA | HEWA |
|---|---|---|
| | | |

c) Taja sifa tatu (3) za maji safi na salama.

i. ______________________________________________

ii. ______________________________________________

iii. ______________________________________________

10. Picha zifuatazo zinaonesha vitendo gani?





i. ____________________________ ii. ____________________________



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org





iii. ________________________ iv. ________________________



v. ________________________________

..............................................



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org